## MAZUNGUMZO



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na viongozi wa Benki ya NMB, wakiongozwa na Ofisa Mtendaji Mkuu, Ruth Zaipuna, Ikulu jijini Dar es Salaam, jana. Picha na Mpigapicha Wetu

UWEZESHAJI

MWANANCHI UK 8.

# *Uvuvi yatengewa Sh29 bil

**Inaelezwa kuwa, kuna utajiri mkubwa kupitia fursa zinazopatikana ukanda wa bahari**

Mwandishi Wetu, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Tanga.** Serikali imetenga Sh29 bilioni katika Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (AFDP) ili kuwezesha kiuchumi shughuli za uvuvi, mikopo kwa wananchi na kukuza pato la Taifa.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega alisema hayo juzi, katika ufunguzi wa kikao kazi cha mkakati na kampeni ya kuhamasisha shughuli za ukuzaji viumbe maji baharini kwa viongozi na wataalamu wa mamlaka za Serikali za mitaa mkoani hapa.

Ulega alisema fedha hizo zimetengwa kwa ajili ya mwaka 2022/23, huku Sh2.1 bilioni zitakopesha wanavikundi vya ufugaji wa samaki, wakulima wa mwani, wafugaji wa majongoo bahari, wanenepeshaji wa kamba koche na kaa katika ukanda wa Bahari ya Hindi.

"Tumekutana wataalamu kupeana mbinu na mikakati ya kuweza kuwafikia wananchi ambao ndio walengwa wakuu wa mradi huu, ili kuona namna tutakavyowainua kiuchumi kupitia fursa zilizoko baharini," alisema Ulega.

Pia, alisema kuna utajiri mkubwa kupitia fursa ya rasilimali zinazopatikana katika ukanda wa bahari, huku Serikali ikidhamiria kuinua hali duni za wananchi waishio ukanda huo.

Ulega aliitaka Benki ya Kilimo kwa kushirikiana na benki nyingine ya biashara kuweka mazingira rafiki ya kutoa mikopo kwa vyama vya ushirika vya vijana na wanawake.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Hashim Mgandilwa alisema changamoto kubwa iliyopo kwa wavuvi wa ukanda huu ni ukosefu wa viwanda na masoko ya uhakika wa mazao ya bahari. Pia, alisema kampeni hiyo italeta chachu na maendeleo ya wananchi watakaopata fursa nyingine ya kiuchumi katika maeneo yao kupitia kilimo cha mwani pamoja na unenepeshaji wa viumbe bahari.

Mwakilishi wa Benki ya Kilimo (TADB), Furaha Sichula alisema kwa mwaka 2021/22 jumla ya Sh4.827 bilioni zilikopeshwa kwenye sekta ya uvuvi ikilinganishwa na mwaka 2020/21 zilikopeshwa Sh1.625 bilioni.

Mkurugenzi wa Ukuzaji Viumbe Maji wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk Nazael Madalla alisema katika mwaka uliopita uzalishaji wa viumbe vya bahari ulikuwa ni asilimia moja pekee.

Alisema kampeni hiyo iliyoanzishwa na Serikali inakwenda kuwasaidia wananchi kujikwamua kiuchumi kupitia fursa za bahari.

# Mo Dewji
# wa 15 ba

Mwandishi Wetu, Mwana
mwananchipapers@mwa

**Dar es Salaam.** Mfany
maarufu Mo ameende
Afrika Mshariki kweny
kung'ara kwenye orodh
Mo, Mtendaji Mkuu
Enterprises (METL), a
mabilionea wa Jarida l
Jarida hilo limemta
15, akifungana na mat
Benjelloun na Youssef
unalingana.
Kwa mujibu wa jarid
kufikia Dola 1.5 bilion
Hata hivyo, licha ya
ameendelea kulinda ut
wa kwa mwaka jana.
Katika orodha ya jari
amejikita kwenye bia
viwanda vya nguo n
nafasi ya 15 akiwa na
Marekani.
* Hata hivyo, uwekez
viwanda vya nguo, ur
ya kupikia, sabuni, su
chanzo cha utajiri wa
Kwa Tanzania Mo
kwenye orodha hiyo
wengine wakitoka Ni
Mo kuingia katika
za mfanyabiashara n
Mamelodi Sundowns
sepe ambaye utajiri
bilioni za Marekani (
Mfanyabiashara Al
amewekeza kwenye
kilichopo Mtwara, a
na utajiri wa Dola 13.
na Johann Rupert n
za Marekani, huku n
Oppenheimer wa A
Dola 8.7 bilioni za M
Kwa miaka kumi i
kupiga hatua kubwa
mabadiliko makubw
shilingi kwenye sek
wa kutimiza ahadi y
ra 100,000 kwa vija
Mo pia amejikita
mwekezaji pekee w
Sh40 bilioni, hivyo

# Washindi tuzo ya Kiswahili kujulikan

Amana Nyembo, Mwananchi
anyembo@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Washindi wa tuzo ya Kiswahili ya Mabati Cornell ya Fasihi ya Afrika ya mwaka 2021 katika utunzi wa riwaya, mashairi na tamthilia kutoka Afrika Mashariki wanatarajiwa kutangazwa kesho.


Tuzo hiyo iliyoanza mwaka 2015 kwa kushirikiana na Taasisi ya Ngugi wa Thiong'o, mshindi wake wa kwanza wa mwaka 2021 atazawadiwa Dola5,000 za Marekani (Sh11,555,000)...

...lenye lengo la kukuza Kiswahili kupitia tanzu hizo.

Alisema washiriki wengi wanatoka Tanzania na Kenya, kwa kuwa ndizo nchi ambazo lugha hiyo imeshika hatamu.

"Mbali na kuwapa zawadi, tumeendelea kushirikiana na washindi watano wa miaka iliyopita kwa kuwasaidia kuchapisha kazi zao Mkuki na Nyota. Lakini tumewawezesha kiuchumi kwa kuwa fedha tunazowapa zinawasaidia kufanya shughuli za Kiswahili, wamekuwa wakiwadhamini wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) wa shahada ya pili ya lugha hiyo na hadi sasa wameshawadhamini wanafunzi sita.

Wadhamini wengine katika tuzo hiyo ni Alaf (Tanzania), Mabati Rollingi Mills (Kenya), Ofisi ya Makamu wa Mkuu wa Masuala ya Kimataifa katika Chuo Kikuu cha Cornell na Idara ya Taaluma za Afrika Chuo Kikuu cha Cornell Marekani



Scanned with CamScanner

* HABARI LEO UK 14.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Farmbase, Suleiman Msellem (kushoto) akitoa maelezo kwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (kulia) kuhusu mchoro wa Kiwanda cha kuzalisha dawa za mifugo kitakachojengwa Wilayani Kigamboni, Mkoa wa Dar es Salaam alipofanya ziara eneo hilo mwishoni mwa wiki. Wengine ni viongozi waandamizi wa serikali na wa kiwanda hicho. (Picha na Wizara ya Mifugo na Uvuvi).

Scanned with CamScanner

Meneja Uzalishaji wa Kiwanda cha Soda cha Anjari kilichopo mkoani Tanga, Safari Mngazija akiwaonesha mabalozi wa kodi jinsi kiwanda hicho kinavyofanya kazi wakati wa ziara yao katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Tanga iliyolenga kuhamasisha wafanyabiashara kulipa kodi kwa hiari na wakati. (Picha na TRA).

HABARI LEO UK 14



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega akizungumza na wataalamu wa sekta za mifugo na uvuvi kuhusu mikakati ya wizara hiyo kabla ya kufungua kikao kazi cha mkakati na kampeni ya kuhamasisha shughuli za ukuzaji viumbe maji baharini kwa viongozi na wataalamu Mkoa wa Tanga. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Hashim Mgandilwa na anayefuata ni Mkuu wa Idara ya Uchumi na Uzalishaji Mkoa wa Tanga, Emigidius Kasunzu. (Picha na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa).

Scanned with CamScanner

## HABARI ZA BIASHARA

HABARI LEO UK 17.

# 'TBA ijitofautishe na wakandarasi wengine'

Na Matem Kayera

KATIBU Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Sekta ya Ujenzi, Balozi Aisha Amour, ameutaka Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kuonesha tofauti katika kazi kati yake na wakandarasi wengine hapa nchini.

Aliyasema hayo alipofanya ziara ya kikazi kwenya Ofisi za Makao Makuu ya TBA Dar es Salaam juzi.

Katika ziara hiyo, Balozi Aisha aliambatana na Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo anayehusika na sekta ya ujenzi, Ludovick Nduhiye.

Ili kuwa na utofauti na wakandarasi wengine, Amour alitaka wakala kufanya kazi kwa weledi zaidi, kuzingatia mikataba na kufanya ubunifu wa majengo unaoendana na wakati.

Pia aliwataka kujenga majengo ya ghorofa mijini, kushirikisha taasisi nyingine zinazotoa huduma za kijamii kama vile maji, umeme na barabara zijue malengo yake ya uendelezaji wa miliki na kuyaingiza kwenye mipango yao ya utekelezaji ili uendelezaji unapofanywa na TBA upate huduma hizo kwa wakati.

Kwa mujibu wa Balozi Aisha, TBA wanapaswa kulinda viwanja na maeneo wanayoyamiliki, kuwa na mpango wa matengenezo wa nyumba zake baina yake na wapangaji wake, kuwa na mpango wa mafunzo kwa watumishi wake hasa kuhusu maadili pamoja na kuendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi.

Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo anayehusika na sekta ya ujenzi, Nduhiye, alipongeza wakala kwa mpango kabambe waliouwasilisha juzi kwa Katibu Mkuu kuhusu mradi wa ujenzi wa nyumba 3,500 za makazi kwa ajili ya watumishi wa umma katika eneo la Nzuguni B jijini Dodoma.

Nduhiye alisema mradi huo utakapokamilika utawasaidia watumishi wa umma kupata makazi bora.

Kwa upande wake, Mtendaji Mkuu wa TBA, Daud Kondoro, alimwahidi Katibu Mkuu kufanyia kazi maelekezo yake ili kuboresha utendaji kazi wa majukumu ya wakala huo.

# Wasindika maziwa Kiteto wapewa somo

Na Mwandishi Wetu

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limetoa mafunzo kwa wasindikaji, wasambazaji na wauzaji wa maziwa na bidhaa za maziwa waliopo katika wilaya za Kiteto (Manyara), Arumeru (Arusha) na Hai (Kilimanjaro) kuhusu kanuni na matakwa ya msingi kuhusu shughuli wanazofanya.

Mafunzo hayo yaliyoanza Januari 17 hadi 25, mwaka huu yamehitimishwa katika Wilaya ya Hai jana mkoani Kilimanjaro yakilenga kuwaelimisha wajasiriamali walio katika mnyororo wa thamani ya ufugaji, ukusanyaji wa maziwa ghafi, ubebaji, usindikaji na bidhaa za maziwa.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo Meneja wa Kanda ya Kaskazini TBS, Happy Kanyeka, alisema wanatambua kuwa sekta hiyo 'ya maziwa ina wajasiriamali wengi wadogo na wa kati ambao husindika na kupeleka sokoni maziwa na bidhaa za maziwa na wengi hufanya hivyo bila kufuata kanuni na taratibu zinazotakiwa.

Kanyeka alisema Kiteto, Arumeru na Hai ni wilaya zinazojihusisha na ufugaji wa ng'ombe wengi wakiwemo wa kienyeji na wa kisasa. Alisema usindikaji wa maziwa na bidhaa za maziwa ni moja ya shughuli zinazofanywa na wajasiriamali katika wilaya hizo.

Akifungua mafunzo hayo juzi, Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Said Irando, aliwataka walengwa wa mafunzo hayo kuzalisha na kusindika maziwa yenye ubora ili kufanikisha azma ya serikali ya kukuza sekta ya viwanda nchini.

"Dhamira ya serikali ni kukuza sekta ya viwanda, hivyo tujibidishe katika kuwekeza kwenye alama ya ubora inayotolewa na TBS kwa kuzalisha na kusindika maziwa yenye ubora ili kutosheleza mahitaji ya soko letu la ndani na hata nje ya nchi," alisema na kuongeza:

"Hilo litawezekana kama tutawatumia wataalamu wetu vizuri, kuzingatia yale wanayotufundisha na kutuelekeza."

Aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kuelewa kwa pamoja kuwa uzalishaji wa maziwa mengi uende sambamba na kukidhi viwango kulinda afya ya mlaji na kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Alifafanua kwamba takwimu za mwaka 2019/2020 zinaonesha uzalishaji wa maziwa ya ng'ombe nchini ni lita bilioni 3.13 kwa mwaka. Kati ya lita bilioni 3.11 (asilimia 99.41) zilizalishwa na wafugaji wadogo na lita milioni 17.8 (asilimia 0.6) zilizalishwa kutoka mashamba makubwa.



Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa ALAF Limited , Hawa Bayumi (katikati) akizungumza na waandishi wa habari kuhusu Tuzo ya Kiswahili ya Mabati-Cornell ya Fasihi ya Afrika itakayofanyika katika ukumbi wa Mlimani City Alhamisi wiki hii. Wengine ni Ofisa Masoko Theresia Mmasy (kushoto) na Sharo Mallya. (Na Mpigapicha Wetu).

# Asiyefanya usafi kutozwa 200,000/-

Na Magnus Mahenge

MKAZI wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma asiyefanya usafi katika makazi yake, kwenye taasisi yake au mahali anapofanyia biashara atatozwa faini kati ya Sh 50,000 na 200,000 au kifungo kisichozidi miezi sita au vyote viwili kwa pamoja.

Mkuu wa Idara ya Mazingira na Udhibiti wa Taka ngumu wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Dickson Kimaro alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa kuhitimisha kampeni ya usafi endelevu katika Kata ya Makole jijini humo.

"Tufanye usafi katika maeneo yetu, tutii sheria bila shuruti kwa sababu sheria ndogo tuliyo nayo katika Jiji la Dodoma inasema mtu asipojitokeza kwenye usafi, mtu asipofanya usafi kwenye eneo lake la makazi, taasisi na biashara, faini yake ni kati ya shilingi 50,000 hadi 200,000 au kifungo kisichozidi miezi sita au vyote viwili kwa pamoja," alisema Kimaro.

Kimaro alisema kampeni hiyo imeanzia katika Kata ya Makole na itaendelea katika kata zote 41 za halmashauri ya jiji hilo, ambaye atashindwa kufanya usafi katika mazingira yake atakumbana na mkono wa sheria hiyo ndogo ya jiji ya kutozwa faini au kifungo.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru alisema ameridhishwa na mwitikio wa wananchi wa Kata ya Makole kushiriki usafi wa mazingira na kuwataka kujenga tabia ya usafi wa mazingira kwa vizazi vijavyo.

Mafuru alisema wananchi wa Dodoma walikuwa wameanza kulegalega kidogo miezi sita iliyopita, hivyo wanatakiwa kurudisha juhudi na tabia hiyo ya kufanya usafi katika maeneo yao.

# ...li North Mara wasifiwa utunzaji mazingira

...wandishi Wetu, ...ma

bayo ni ubia baina ya Barrick na Serikali ya Tanzania.

jachukuliwa na Barrick. Alisema awali kulikuwa...

mgodi, hii ni habari njema

zimepungua hadi kufikia

ilikuwa maalumu kwa...

Scanned with CamScanner

zania wengi wanaishi.

"TCB sio kwamba tu ni benki kubwa nchini, bali pia inatoa mchango mkubwa katika shughuli za kijamii hasa kuinua viwango vya elimu pamoja na upatikanaji wa huduma bora za afya," alisisitiza.

Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mrindoko, aliipongeza benki hiyo kwa uwekezaji huo, akisema utakuwa wa manufaa kiuchumi na kifedha na kwamba umekuja wakati muafaka,

"Huduma za kibenki zinahitajika mkoani humu kwa muda mrefu sasa, uwepo wa tawi hili kutaongeza idadi ya wananchi wenye akaunti za benki kitu ambacho ni muhimu kwenye maendeleo ya huduma jumuishi za fedha na shughuli za uzalishaji kwa ujumla," alisema Mrindoko.

"Katavi ni mkoa tajiri uliojaliwa rasilimali nyingi kwa hiyo uwepo wa huduma za kibenki za uhakika ni suala muhimu sana kwa ajili ya maendeleo."

# Machinjio sasa kuanza uchinjaji ng'ombe 100, mbuzi 1,000 kila siku

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

NIPASHE UK 7

MACHINJIO ya kisasa ya mifugo ya Nguru Hills Ranch Ltd yenye uwezo wa kuchinja ng'ombe 100 na mbuzi 1,000 kwa siku yaliyoko wilayani Mvomero Mkoa wa Morogoro yanatarajiwa kuanza rasmi Machi mosi, mwaka huu, hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi na ajira.

Mkurugenzi wa Mipango na Uwekezaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa watumishi wa Umma (PSSSF ), Fortunatus Magambo, alibainisha hayo kwa wahariri kutoka vyombo vya habari waliofanya ziara ya kutembelea na kujionea maendeleo ya mradi wa machinjio ya kisasa.

Alisema mradi huo wa machinjio hayo unamilikiwa kwa ubia kati ya Serikali kupitia Mfuko wa PSSSF , Eclipse Investiment (LLC) na Kampuni ya Busara Investiment (LLP).

Alisema mradi huo ulianza mwaka 2018, lakini ugonjwa wa Covid -19 ulipoanza ulisababisha mashine zilizoagizwa kutoka nje kuchelewa kuletwa pamoja na wataalamu wake hadi Julai mwaka jana zilipoletwa na kuanza kufungwa na kwamba kazi hiyo ipo kwenye hatua ya mwisho.

Naye Meneja Uhusiano na Elimu kwa wanachama PSSF, James Mlowe, alivitaka vyombo vya habari kuunganisha jamii, Serikali na wadau wa maendeleo katika utoaji wa taarifa sahihi katika uhamasishaji wa kukuza uchumi na maendeleo ya watu.

Mlowe alisema kuwa mfumo wa PSSF umewekeza katika kiwanda hicho wa asilimia 30,ikiwa ni sehemu ya mkakati wake katika uwekezaji wa miradi mbalimbali hasa katika kipindi hiki ambacho taifa limejiwekeza katika uchumi wa viwanda.

Scanned with CamScanner

>>Idadi ya wanafunzi waliofaulu kidato cha kwanza Kilosa

# ;433 wakacha kidato cha kwanza Kilosa

;A

ı Kilosa,
, Majıd
nesema
6,433
la saba
a shule
ɔ cha

katika
akuyo,
a Rais
ıkisha
shule
gaji.
ıi ya
ıdato
ılımia
ı kwa

wilaya hiyo wanatakiwa kuanza shule ni 9,942.

Aliwataka wazazi na walezi wenye watoto waliofaulu waripoti shuleni kuendelea na masomo ya sekondari kwa sababu ya serikali imetoa fedha kuboresha miundombinu ya elimu kwa kujenga wa vyumba vya madarasa.

"Kati ya watoto waliofaulu asilimia 66 hawajaripoti shuleni kuanza kidato cha kwanza hadi leo, niwaombe wazazi kuhakikisha wote wanaotakiwa kuripoti shule waanze mara moja na kuwasimamia hadi watakapo maliza shule,"alisema.

Mwanga alisema katika kuhakikisha watoto wote wanapata haki ya elimu, wameweka utaratibu wa kila mzazi kutia saini mkataba wa miaka minne wa kumpeleka mwanafunzi shule na kumsimamia kwa kipindi chote cha masomo.

Alisema pamoja na mambo mengine, mkataba huo umelenga kuwabana wazazi ambao hukatisha masomo ya watoto wao kwa sababu zisizokuwa za msingi zikiwemo kuwaozesha wakiwa wadogo au kuwapa kazi za kuchunga mifugo.

Chifu wa Kabila la Kimasai wa Jamii ya Parakuyo, Kashu Moreto, alimshukuru Rais Samia kuwapatia vyumba vya madarasa ili watoto wao wapate elimu kama ilivyo kwa jamii nyingine.

Alisema awali walikuwa wakikabiliwa na changamoto ya uhaba wa vyumba vya madarasa kwa sababu ya dhana iliyojengeka kuwa wafugaji hawazingatii elimu ya watoto wao.



# ufisadi kitengo cha leseni

67,8 zilizokusanywa za ulipaji wa leseni hazijulikani zilipo.

"Shilingi milioni 100.8 zilizokusanywa kwa kipindi cha 2020/2021 za leseni pia hazijulikani zilipo na shilingi milioni 1.3 a malipo ya leseni zilizokusanywa kati a Julai mwaka jana hazijulikani zilipo," lieleza Mbuge.

Alisema kiasi hicho cha fedha ni kubwa ambapo kama kingeingizwa ıtika mfumo wa serikali kingeleta aendeleo ya wananchi wa Bukoba.

"Katika uchunguzi huo wa awali eonekana kuna kampuni ya utafiti EDI ililipia sh. milioni 4.5 kwa ajili ya eni B 03292344 ya mwaka 2019 hadi 20 lakini kwenye mfumo wa mapato halmashauri haionekani," alieleza.

Alitaja leseni nyingine yenye namba 528011 ya shule ya Adroph Kolping lish medium ambayo ililipwa sh. oni 1.2 lakini fedha inayoonekana kuingizwa katika mfumo ni sh. laki sita.

"Pia katika uchunguzi huo imebainika leseni nyingi za wafanyabiashara wa Manispaa ya Bukoba ni feki, hivyo nimeagiza tuletewe majina ya wafanyabiashara wa wilaya zote za mkoa huu," aliagiza.

Alisema kutokana na uchunguzi huo wa awali uliofanywa na tume hiyo iliyosimamiwa na Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, Moses Machali na kubaini mapungufu hayo, ameikabidhi ripoti ya tume hiyo kwa uongozi wa TAKUKURU ili kufanya uchunguzi.

Machali alisema tume hiyo imefanya kazi kwa muda wa wiki tatu ambapo walibaini sh. milioni 171.8 za leseni hazionekani katika mtandao na sh. milioni 156 zinazoonekana kwenye vitabu vya stakabadhi bado zinafuatiliwa kuona ziliingizwa wapi.

# Serikali yatoa mabilioni kuboresha sekta ya uvuvi

NA SCOLASTICA MSEWA, TANGA

SERIKALI ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, imetenga sh. bilioni 29 kuwezesha shughuli za uvuvi kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (AFDP).

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, aliyasema hayo juzi, wakati wa ufunguzi wa kikao kazi cha mkakati na kampeni ya kuhamasisha shughuli za ukuzaji viumbe maji wa bahari kwa viongozi na wataalamu wa mamlaka za serikali za mitaa mkoani Tanga.

Alifafanua kuwa sehemu ya fedha hizo sh. bilioni 2.1 zinakwenda kukopeshwa kwa vikundi vya wafugaji wa samaki, wakulima wa mwani, wafugaji wa jongoo bahari, wanenepeshaji kamba kochi na kaa, katika ukanda wa Bahari ya Hindi.

**"Tumekutana na wataalamu kupeana mbinu na mikakati ya kuwafikia wananchi ambao ndiyo walengwa wakuu wa mradi huo ili kuona namna ambavyo tutawainua kiuchumi kupitia fursa zilizopo baharini".**

**Abdallah Ulega**

"Tumekutana na wataalamu kupeana mbinu na mikakati ya kuwafikia wananchi ambao ndiyo walengwa wakuu wa mradi huo ili kuona namna ambavyo tutawainua kiuchumi kupitia fursa zilizopo baharini," alisema.

Ulega alisema kuna utajiri kupitia fursa ya rasilimali zinazopatikana katika ukanda huo, hivyo serikali imedhamiria kuinua hali duni za wananchi waishio katika ukanda wa pwani.

Aliongeza Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) na benki zingine za biashara, ziweke mazingira rafiki ya kutoa mikopo kwa vyama vya ushirika ili vifanye shughuli za kunenepesha kaa, kamba kochi, ufugaji wa samaki, jongoo bahari na kilimo cha mwani.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Hashim Mgandilwa, alisema changamoto iliyopo kwa wavuvi wa ukanda huo ni ukosefu wa viwanda na masoko ya uhakika ya mazao ya bahari.

Alisema kampeni hiyo italeta chachu na maendeleo ya wananchi kwa kuwa watapata fursa nyingine ya kiuchumi katika maeneo yao kupitia kilimo cha mwani na unenepeshaji wa viumbe bahari.

Naye, mwakilishi kutoka TADB, Furaha Sichula, alisema mwaka 2021/2022 sh. bilioni 4.8 zimekopeshwa katika sekta ya uvuvi ikilinganishwa na mwaka 2020/2021 ambapo sh. bilioni 1.6 zilikopeshwa.

Mkurugenzi wa ukuzaji viumbe maji kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Nazael Madalla, alisema katika mwaka uliopita uzalishaji wa viumbe vya bahari ulikuwa ni asilimia 11 pekee.

Scanned with CamScanner